

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam.
Tarehe 4 Machi 2007**

Waliohudhuria

Elaine Baker
Juma Ali Salehe Jongo
Selemani Alonasi
Shukuru Hassan

Elaine aliripoti kuwa yeye, Mejah na Sostenes walihudhuria Jukwaa la jamii la kidunia Nairobi Kenya, Januari kwa hiari yao kama wanachama wa UWABA na wanachama wa kundi jingine. Ilikuwa ni ujuzi wa kipekee uliowawezesha kujua mengi kuhusu masuala ya kijamii. Aliripoti kwamba kampeni na uwakilishi wa makundi Nairobi ulikuwa mzuri, makundi yaliwakilisha wachuuzi wa matunda, wapanda baiskeli/pikipiki wa boda-boda n.k.

Elaine aliripoti kuwa UWABA imepeleka barua Mlimani City, kituo cha biashara, karibu na Mwenge, kulalamika kuwa hawakuweke maegesho ya baiskeli tu ila pia hawaruhusu baiskeli kuingia eneo hilo. Hii ni licha ukweli kuwa yapo maduka yanayouza baiskeli na vifaa vyake humo. Mejah alipeleka barua hiyo kwa uongozi, na kutaka kuonana na meneja ila hakuwepo.

Elaine aliripoti kuwa UWABA imepeleka barua kwa Waziri wa Miundombinu Ndugu Andrew Chenge ili kufanya nae kikao. Katibu muhtasi alimpigia Mejah na kumwambia kuwa Waziri ameisoma na majibu yangetumwa. Mejah alitakiwa kwenda kuangalia sanduku la barua. Inatumainiwa kuwa UWABA itakutana na waziri na tutajumuishwa kwenye mjadala na TANROADS iwapo waziri atasaidia ushiriki wetu.

TANROADS hawajajibu barua yetu ya kuomba nafasi katika barabara ya Sam Nujoma licha ya kuahidi kufanya hivyo kwenye mkutano wa Mei. Elaine aliahidi kuwapigia simu wiki itakayofuata kwa ufuatiliaji.

Kikao kilipitia mada zilizotolewa na TANROADS na kurekebisha ili kutolewa kwa Waziri. Ilikubalika kupeleka barua polisi kuomba idadi ya ajali zilizowaathiri wapanda baiskeli. Kikundi kiliandika barua na Juma alisema angeipeleka wiki inayofuata.